
Nipashe MWANGA WA JAMII
Jumanne Agosti 4, 2026






Dereva wa bodaboda akishafirisha mzigo unaozidi uwezo wa pikipiki, eneo la Goba Dar es Salaam juzi, kitendo kinachohatarisha usalama barabarani. **PICHA: SABATO KASIKA**

Nipashe MWANGA WA JAMII
Jumanne Agosti 4, 2026



MABASI YALIYOGONGANA:

# Idadi ya vifo yaongezeka ajali ya Dodoma, dereva ashikiliwa

Na Rehema Matowo, DODOMA
0715086344 WhatsAPP SMS

JESHI la Polisi Mkoa wa Dodoma linamshikilia dereva wa basi la Isamilo Express kwa tuhuma za kusababisha ajali ya barabarani iliyohusisha mabasi mawili kugongana uso kwa uso katika Kijiji cha Ibihwa, wilayani Bahi na kusababisha vifo vya watu tisa pamoja na majeruhi 65.

Kwa mujibu wa uchunguzi wa awali wa polisi, ajali hiyo ilitokana na uzembe wa dereva wa basi la Isamilo Express aliyedaiwa kuyapita magari yaliyokuwa mbele yake bila kuhakikisha njia ilikuwa salama, hatua iliyosababisha kugongana uso kwa uso na basi la Libanika Luxury lililokuwa likitokea upande wa pili.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Gallus Hyera, alisema jana kuwa dereva huyo anaendelea kushikiliwa huku uchunguzi ukiendelea na taratibu za kisheria zikichukuliwa.

Alisema hadi sasa watu tisa wamefariki dunia, wakiwamo wanaume watano na wanawake wanne, huku majeruhi wengine wakipatiwa matibabu katika hospitali mbalimbali.

"Uchunguzi wa awali unaonesha kuwa dereva wa basi la Isamilo Express lenye namba za usajili T 428 EPX, lililokuwa likitoka Mwanza kuelekea Dar es Salaam, alisababisha ajali hiyo baada ya kuyapita magari yaliyokuwa mbele yake bila kuchukua tahadhari na kugongana uso kwa uso na basi la Libanika Luxury lenye namba T 897 DUP lililokuwa likitoka Dar es Salaam kuelekea Mwanza," Kamanda Hyera alisema.

Aliongeza kuwa kati ya majeruhi hao, watu tisa wako katika hali mbaya zaidi na wanaendelea kupatiwa matibabu chini ya uangalizi wa madaktari, huku wengine wakipata majeraha madogo pamoja na mshtuko kutokana na tukio hilo.

Miili ya waliofariki dunia imehifadhiwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma na Kituo cha Afya Makole kwa ajili ya utambuzi na taratibu nyingine.

Baadhi ya manusura wa ajali hiyo walisema walikuwa wameanza kuhofia mwenendo wa safari muda mfupi kabla ya ajali kutokana na mwendo kasi wa basi la Isamilo Express.

Mmoja wa majeruhi, Yassin Nyalusi, mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) aliyekuwa akisafiri kuelekea Mwanza, alisema baadhi ya abiria walimwonya dereva kupunguza mwendo, lakini madai yao hayakuzingatiwa.

"Saa 12 asubuhi nilishangaa kuona basi likihama kutoka upande wake na kuingia upande tuliokuwa tunapita. Baada ya hapo yakagongana uso kwa uso," alisema.

Kauli za mashuhuda hao zinaendelea kufanyiwa kazi na vyombo vya uchunguzi ili kubaini mlolongo kamili wa tukio hilo.

Jeshi la Polisi limewataka madereva wote kuzingatia sheria za usalama barabarani, hasa wakati wa kuyapita magari mengine, kwa kuhakikisha kwanza kuwa njia ni salama na hakuna hatari ya kugongana na magari yanayotoka upande wa pili.

Pia limewakumbusha abiria umuhimu wa kufunga mikanda ya usalama wakati wote wa safari, likieleza kuwa hatua hiyo inaweza kupunguza ukubwa wa majeraha endapo ajali itatokea.

Kamanda Hyera alisema uzembe wa madereva unaendelea kuwa miongoni mwa sababu kuu za ajali nyingi za barabarani nchini na kusababisha vifo, ulemavu wa kudumu pamoja na hasara kubwa za kiuchumi na kijamii.

Ajali hiyo imeibua tena mjadala kuhusu umuhimu wa kuimarisha nidhamu ya madereva na utekelezaji sheria za usalama barabarani.

Sheria ya Usalama Barabarani, Sura ya 168, pamoja na kanuni zake, zinawataka madereva kuendesha vyombo vya moto kwa uangalifu, kuzingatia alama za barabarani, kutokufanya mwendo wa hatari na kuhakikisha wanafanya uamuzi salama wanapoyapita magari mengine.

Vilevile, Sera ya Taifa ya Usalama Barabarani inalenga kupunguza vifo na majeruhi vinavyotokana na ajali kwa kuimarisha elimu kwa watumiaji wa barabara, usimamizi wa sheria na uwajibikaji wa wadau wote wa sekta ya usafiri.

Katika ngazi ya kimataifa, Malengo ya Maehdeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa (SDG 3.6) yanazitaka nchi kupunguza kwa kiasi kikubwa vifo na majeruhi vinavyotokana na ajali za barabarani kupitia usimamizi madhubuti wa usalama wa usafiri.

Mpango wa Kimataifa wa Muongo wa Hatua za Usalama Barabarani 2021-2030 unaoratibiwa na Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO) na Umoja wa Mataifa (UN) unasisitiza kuimarishwa kwa nidhamu ya madereva, matumizi ya mikanda ya usalama, utekelezaji sheria na usimamizi wa mwendo kasi kama njia muhimu za kuokoa maisha.

